

## **JINSI KITUO CHA KUDHIBITI VIUMBE HAI WAHARIBIFU KINAVYOKUZA VIPAJI VYA VIJANA KUINUA TAFITI HAPA NCHINI**

*Na, Francis Mwakatanya*

Kituo cha Kudhibiti Viumbe hai Waharibifu cha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, SUA, kimefanikiwa kuanzisha programu mahususi ya kuibua na kulea watafiti chipukizi nchini ‘Early Career Researchers Development Program’.

Akiongelea kuhusu programu hiyo Mkurugenzi wa Kituo hicho, Bw. Ladslaus Mnyone alibainisha kuwa kituo kimeanzisha programu hii ili kuongeza idadi ya wanasayansi wabobezi katika tafiti zinazolenga kuboresha udhibiti wa viumbe hai wanaoathiri kilimo, mifugo na afya ya jamii.

Viumbe hao ni kama vile panya, ndege, viwavi jeshi, voroboto, mbu, kunguni, mbung'o, mende, papasi, kupe na wengineo, Aidhakituo kinatarajia kuongeza wabobezi katika tafiti zinazolenga kubaini faida za baadhi ya viumbe hao kama vile matumizi ya panyabuku kutambua vimelea wa magonjwa ya mimea, mifugo na binadamu.

Watafiti chipukizi wanatokana na wahitimu wa shahada za awali katika kilimo, mifugo, afya ya jamii na nyanja mtambuka za sayansi, teknolojia na ubunifu kwa mfano tehama na intelijensia bandia ‘artificial intelligence’.

Baada ya kujiunga, watafiti hao wanapata fursa ya kujifunza na kupata uzoefu kupitia wanasayansi wabobezi waliopo ndani ya kituo na vyuo au taasisi washirika, ndani na nje ya Tanzania, aidha, watafiti chipukizi wanajengewa uwezo kwa kupitia njia mbalimbali kama vile kushiriki kwenye tafiti zilizopo, kuandaa mapendekezo ya tafiti ‘Grant research proposals’, mafunzo ya darasani, safari za mafunzo mahususi kupitia taasisi washirika ndani na nje ya Tanzania na kutafutiwa ufadhili wa masomo ya shahada za umahiri na uzamivu kupitia wanasayansi waandamizi ndani ya kituo na taasisi washirika.

Programu ya kuibua na kulea watafiti chipukizi ilianza Agosti, 2017 ikiwa na wanafunzi sita (6) hadi kufikia mwezi wa Machi, 2020, programu hii ina idadi ya wanafunzi kumi na tatu (13).

Bw. Mnyone aliendelea kusema kuwa watafiti watatu (3) kati ya hao wameshapata ufadhilli na kuanza masomo ya shahada za umahiri kupitia miradi miwili ya utafiti inayofadhiliwa na Serikali ya Tanzania kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia nchini (COSTECH), na Serikali ya Sweden kupitia ‘Swedish International Development Cooperation Agency’ mradi wa pili unaendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi ya Afya ya Ifakara pamoja na Chuo Kikuu cha Sayansi za Kilimo cha nchini Swiden.

Bw. Mnyone anasema kuwa kituo kupitia programu hiyo kitawezeka kuwaandaa vijana wa kitanzania kwenye ushindani wa soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Pia kwa kupitia ongezeko la miradi ya utafiti ndani ya kituo na chuo kwa ujumla, baadhi ya watafiti katika programu hii wataajiriwa kupitia miradi hiyo. “Azma yetu ni kuajiri rasilimali watu yakutosha kwa kupitia miradi ya utafiti na vyanzo vinginevyo ili kuongeza kasi na ubora wa tafiti zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali za nchi yetu. Kwa kutambua kwamba serikali pekee haiwezi kutoa ajira kwa idadi tunayohitaji kutokana na wingi wa majukumu yake hivyo tumenuia kwa dhati kabisa kuongeza ajira za mikataba kwa kupitia miradi ya utafiti” alisisitiza Bw. Mnyone.

Kituo kwa sasa kimeshaanza kuwasiliana na makampuni , Taasisi za serikali na mashirika mbalimbali ili kuona uwezekano wa kupata fursa ya watafiti chipukizi kufanya kazi kwenye maeneo hayo kwa kipindi kisochopungua miezi sita ili kubaini changamoto na fursa zilizopo na kisha kuzitafuta ufumbuzi kwa kupitia tafiti na ubunifu; kwa matarajio kwamba matokeo chanya ya tafiti hizo yatachangia katika kuunga mkono serikali ya awamu ya tano na zijazo katika sekta ya viwanda.

Hadi sasa kituo kinapokea maombi mengi kutoka kwa wahitimu kutoka vyuo mbalimbali nchini ili kujiunga na programu hii isipokuwa uwezo wa kituo kwa sasa ni kupokea wanafunzi watatu (3) hadi watano (5) kutokana na rasilimali chache. Iwapo mazingira yataruhusu lengo letu ni kuchukua wahitimu nane (8) hadi kumi(10 )kwa mwaka ambaa wataendelea kuchujwa kila baada ya miezi mitatu.

Hivyo, ili kituo kiweze kupokea wahitimu wengi kwa wakati husika, hasahasa katika kipindi hiki cha mpito, kinahitaji kuboresha na kuongeza vyumba viwili (2) vikubwa vya ofisi, vyumba na vifaa vya maabara, na fedha kwa ajili ya safari za mafunzo ndani na nje ya nchi . Kwa hiyo Mkurugenzi wa kituo hicho anakaribisha michango ya hali na mali ili kusaidia programu hii iweze kunufaisha vijana wengi na kuongeza mchango wa utafiti katika kasi ya ukuaji wa uchumi.